# Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 DESEMBA, 2025

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusinimagharibi na maeneo jirani, hali ambayo iliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Vile vile, uwepo wa upepo wenye unyevunyevu uvumao kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani uliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo hasa katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi. Pia, vipindi vya mvua katika maeneo machache ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 DESEMBA, 2025

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 DESEMBA, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusinimagharibi na maeneo

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

jirani, hali ambayo inatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Vile vile, uwepo wa upepo wenye unyevunyevu uvumao kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu unatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo hasa katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 DESEMBA, 2025**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache ya mikoa ya Kigoma na Katavi hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwisho.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***